

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1

Fax Nam. + 255 24 2230215

Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz



SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR

Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU TAARIFA YA SERIKALI KUHUSU HOJA YA UDANGANYIFU NA KUJIPATIA FEDHA KWA MFANYAKAZI WA KITENGO CHA DAMU SALAMA

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa katika Mkutano huu wa Nne wa Baraza la Kumi katika hali ya uzima wa afya, amani na utulivu na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kukidhi matakwa ya kanuni ya 44(3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 ya kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na **Taarifa ya Serikali Kuhusu Hoja ya Udanganyifu na Kujipatia Fedha kwa Mfanyakazi wa Kitengo cha Damu Salama.**

Mheshimiwa Spika, Hoja hii ilitolewa na Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo, Mheshimiwa Hamza Hassan Juma katika Mkutano wa Tatu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika kikao kilichofanyika tarehe 28 Mei, 2021 ambapo alitoa Hoja ya Kuundwa kwa Kamati Teule kwa ajili kufuatilia tuhuma za mtumishi wa Kitengo cha Benki ya Damu Salama kuchangisha fedha na vifaa kwa ajili ya matumizi ya Kitengo cha Damu Salama kinyume na utaratibu na kutumia vibaya nembo ya Serikali kwa nia ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, pia, sina budi kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutimiza ahadi yake ya kuifanyia kazi hoja hii na kuwasilisha Taarifa yake katika Mkutano huu wa Nne.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwatambulisha Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Hassan Khamis Hafidh Mwenyekiti
2. Mhe. Mtumwa Peza Yussuf Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Machano Othman Said Mjumbe
4. Mhe. Suleiman Makame Ali Mjumbe
5. Mhe. Salma Mussa Bilal Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha Mjumbe
7. Mhe. Zaina Abdalla Salum Mjumbe

- | | | |
|-----|------------------------|-----------|
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| 9. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilikutana na kuijadili taarifa hii na kukubaliana mambo yafuatayo:

(a) Kamati imebaini kukosekana kwa utaratibu wa kutekeleza jambo hili katika hatua za awali ndani ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto;

(b) Kamati imebaini kuwa Kamati iliyoundwa na Serikali bado haijakamilisha uchunguzi wa jambo hili. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zifuatazo kuendelea kukamilisha uchunguzi na taarifa ya uchunguzi huo iwasilishwe katika Mkutano wa Tano wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Taasisi zenyewe ni:

- (i) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (ZAECA),
- (ii) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii na nawaomba Wajumbe wa Baraza hili kutoa michango yao juu ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Naomba Kuwasilisha.

.....

(Mtumwa Peya Yussuf)

Makamu Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

Baraza la Wawakilishi Zanzibar